AFRICAN UNION

الاتحاد الأفريقي

UMOJA WA AFRIKA

UNION AFRICAINE

UNIÃO AFRICANA

UNIÓN AFRICANA

Addis Ababa, Ethiopia S.L.P 3243 Simu: +251 115 517 700 Nukushi: +251 115 517 844
Tuvuti: www.au.int

BARAZA KUU
Mkutano wa Arobaini na Nne wa Kawaida
Tarehe 14 - 15 Februari 2024
Addis Ababa (Ethiopia)

EX.CL/1514(XLIV)
Matini chanzi: Kiingereza

RIPOTI YA UCHAGUZI NA UTEUZI WA MWANACHAMA MMOJA (1) WA TUME YA UMOJA WA AFRIKA YA SHERIA ZA KIMATAIFA (AUCIL)

RIPOTI YA UCHAGUZI NA UTEUZI WA MWANACHAMA MMOJA (1) WA TUME YA UMOJA WA AFRIKA YA SHERIA YA KIMATAIFA (AUCIL)

1. Uchaguzi wa wanachama wa Tume ya Umoja wa Afrika ya Sheria za Kimataifa (AUCIL) unaongozwa na vifungu vya Katiba ya AUCIL (Katiba) na Kanuni za Utaratibu wa Baraza Kuu.

2. AUCIL ilianzishwa kufuatana na Ibara 5(2) ya Sheria ya Kuanzisha Umoja wa Afrika kama chombo cha ushauri wa AU.

3. Ibara ya 3 ya Katiba inabainisha kwamba AUCIL itajumuisha wanachama kumi na moja (11), ambao wana "uwezo uliokubalika katika sheria ya kimataifa, ambao ni raia wa Nchi Wanachama na ambao watatumikia kwa uwezo wao binafsi."

4. Zaidi, Ibara ya 3(2) ya Katiba inaeleza kwamba AUCIL haitajumuisha zaidi ya mwanachama mmoja (1) kutoka nchi moja.

5. Ibara za 11 na 12(2) za Katiba zinabainisha kwamba wanachama wa AUCIL wanachaguliwa na Baraza Kuu kwa kupiga kura ya siri kwa kipindi cha miaka mitano (5) na wanastahili kuchaguliwa tena mara moja tu.

6. Inakumbukwa kwamba Bi. Tomassa Bisia ELA NCHAMA, kutoka Guinea ya Ikweta aliteuliwa kuwa mwanachama wa AUCIL mwezi Februari, 2019 kwa kipindi cha miaka mitano (5), kufuatana na vifungu vya Ibara za 11 na 12 za Katiba. Hivyo basi, muda wake wa kuhudumu utamalizika mwezi Februari 2024.

7. Mwanachama anayemaliza muda wake ana sifa ya kuchaguliwa tena.

Taratibu za Uchaguzi

8. Kifungu cha 2 cha Uamuzi EX.CL/907(XXVII) kuhusu Taratibu za Kutekeleza Vigezo vya Uwakilishi wa Haki wa Kijiografia na Jinsia Katika Vyombo na Taasisi za Umoja wa Afrika, uliopitishwa na Baraza Kuu mwezi Januari 2016, kinaeleza kama ifuatavyo:

i) Uwakilishi wa kikanda, pale unapofaa, utakuwa Mashariki (2), Kati (2), Kaskazini (2), Kusini (2) na Magharibi (2), isipokuwa katika hali ambapo eneo ambalo limearifiwa vyema halijawasilisha wagombea;

ii) Pale inapofaa, kiti kimoja (1) kitakuwa kiti kinachoelea na kitazunguka kati ya kanda tano (5);

iii) Angalau mwanachama mmoja (1) kutoka kila kanda lazima awe mwanamke;

iv) Taratibu hizi zitaanza kutekelezwa mara moja.

9. Kutokana na hayo, uwakilishi wa kikanda na kijinsia wa AUCIL baada ya kumalizika kwa muda wa mwanachama mmoja (1) utakuwa kama ifuatavyo:

KANDA	**WANACHAMA**	**JINSIA**	
		MWANAMKE	**MWANAUME**
Kati	2 (mmoja akikalia kiti kinachozunguka) [1]	0	2
Mashariki	2	1	1
Kaskazini	2	1	1
Kusini	2	1	1
Magharibi	2	1	1
JUMLA	**10**	**4**	**6**

10. Kuhusiana na hilo, kwa kuzingatia Taratibu za Kutekeleza Vigezo vya Uwakilishi wa Haki Kijiografia na Jinsia katika Vyombo vya Umoja wa Afrika, wanachama wafuatao watateuliwa:

- **Kanda ya Kati: Mgombea mmoja mwanammke**

<u>Uwasilishaji wa wagombea</u>

11. Kamisheni, kupitia Barua yenye kumbukumbu namba BC/OLC/42.23/13703.23 iliyotolewa tarehe 30 Agosti, 2023, ilizialika Nchi Wanachama kuwasilisha wagombea kabla ya muda wa mwisho tarehe 30 Oktoba, 2023.

12. Aidha, Kamisheni, kupitia Barua yenye kumbukumbu namba BC/OLC/ 23.21B/ 42.23/13860.23 iliyotolewa tarehe 13 Oktoba, 2023 ilizikumbusha Nchi Wanachama kuhusu uchaguzi na muda uliowekwa.

13. Wagombea waliopokelewa kutoka Nchi Wanachama ni kama ifuatavyo:

No.	**JINA**	**JINSIA**	**NCHI**	**KANDA**	**MAONI**
1	Ms. Tomassa Bisia **ELA NCHAMA**	Mwanamke	Guinea ya Ikweta	Kati	Anastahili kuchaguliwa tena

[1] Kiti kinachozunguka kwa sasa kinakaliwa na Bw. Alain Didier OLINGA, mwanamume kutoka Cameroon, aliyechaguliwa kwa kipindi cha miaka mitano mwezi Julai 2023.

Uteuzi

14. Itakumbukwa kwamba Mkutano Mkuu kupitia Uamuzi wa Mkutano wa AU/AU/Dec.760(XXXIII) uliopitishwa mwezi Februari 2020 huko Addis Ababa, Ethiopia, lilikabidhi mamlaka yake ya uteuzi wa wanachama wa baadhi ya Vyombo na Taasisi za AU, ikiwa ni pamoja na AUCIL, kwa Baraza Kuu.

15. Kuhusiana na hilo, mwanachama aliyechaguliwa atateuliwa moja kwa moja na kwa wakati mmoja na Baraza Kuu

RASIMU YA UAMUZI NA UCHAGUZI WA MWANACHAMA MMOJA (1) WA TUME YA SHERIA ZA KIMATAIFA WA UMOJA WA AFRIKA (AUCIL)

Baraza Kuu,

1. **LINAKUBALI Ripoti** ya Kamisheni kuhusu Uchaguzi na Uteuzi wa Mwanachama Mmoja (1) wa Tume ya Umoja wa Afrika ya Sheria ya Kimataifa (AUCIL);

2. **LINACHAGUA na KUTEUA mwanachama wa AUCIL kwa kipindi cha miaka mitano (5) kama ifuatavyo:**

NO.	JINA	JINSIA	NCHI	KANDA
1				

AFRICAN UNION UNION AFRICAINE

African Union Common Repository **http://archives.au.int**

Organs Council of Ministers & Executive Council Collection

2024-01-15

Report on the Election and Appointment of One (1) Member of the African Union Commission on International Law (AUCIL)

African Union

African Union

https://archives.au.int/handle/123456789/10548

Downloaded from African Union Common Repository